TANGAZO LA SERIKALI NA.192 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA KITISI YA MWAKA 2022.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Kitisi ya Mwaka 2022.

Kutangaza Eneo la Upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipangokina katika eneo la kwenye Jedwali utaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye njiapanda ya barabara ya Njombe – Songea na bomba la mafuta la Tanzania - Zambia - Mafuta (TAZAMA) kwenye alama yenye majira – nukta 700553MS, 9021369KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Njombe – Songea kwa umbali wa kilomita 1.633 hadi eneo ambalo barabara za Njombe – Songea na Dar Es Salaam – Mbeya zinapokutana kwenye majira – nukta 700394MS, 9019778KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya Dar es Salaam – Mbeya hadi jengo la Ofisi ya Mtaa wa Kahawa kwa umbali wa kilomita 0.614 hadi kwenye majira – nukta 699836MS, 9020035KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi kwa kufuata barabara ya Kabelege hadi barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa kwa umbali wa kilomita 0.324 hadi kwenye majira - nukta 699594MS, 9019818KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa na kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.667 hadi kwenye majira - nukta 699190MS, 9020341KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa kwa umbali wa kilomita 1.583 hadi bomba la mafuta la TAZAMA kwenye majira – nukta 699399MS, 9021911KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata bomba la mafuta la TAZAMA kwa umbali wa kilomita 1.227 hadi ulipoanzia".

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINA S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*